

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

Simu Na: +255 (026) 2963630  
Nukushi: +255 (026) 2963629  
Barua Pepe: [ps@utumishi.go.tz](mailto:ps@utumishi.go.tz)  
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Utumishi,  
S.L.P 670,  
**DODOMA.**

**Mtumba, DODOMA**  
**Tarehe 31 Disemba, 2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kumekuwa na taarifa ya upotoshaji inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kutolewa kwenye mifumo ya kiutumishi ukiwemo Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) watumishi wenye mkanganyiko wa majina na umri katika mfumo huo.

Wapotoshaji hao wamekuwa wakiwapigia simu baadhi ya watumishi na kuwaeleza kuwa Serikali imewaelekeza kufanya uhakiki wa taarifa za watumishi hao kwenye mfumo wa LAWSON na kubaini kuwa kuna mkanganyiko wa taarifa zao, hivyo wamewaondoa kwenye mfumo huo na kwamba mwezi Januari, 2024, hawatopata mshahara.

Wapotoshaji hao wamekuwa wakitumia simu za mkononi zenye namba 0768003548, 0749633210 na 0683377133 kuwapigia watumishi hao na wakati mwingine kutaka fedha toka kwao ili wawasaidie.

Taarifa hizo zimezua taharuki na kuleta usumbufu mkubwa kwa watumishi wa umma nchini.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inawasisitiza Watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla kuwa makini na taarifa za namna hiyo zinazotolewa na zitakazoendelea kutolewa kwani Serikali ina utaratibu wake wa kutoa taarifa kwa wadau wake na sio utaratibu unaotumika na wapotoshaji hao.

Aidha, Mfumo wa LAWSON unaotajwa na wapotoshaji hao haupo kwa sasa na hautumiki kabisa Serikalini.

Ofisi inatoa onyo kali kwa wapotoshaji hao na kuacha tabia hiyo kwani kupitia vyombo yake vya dola inafuatilia nyendo zao ili kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.

A handwritten signature in blue ink that reads "Mary L. Mwakapenda".

Mary L. Mwakapenda  
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**